**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents | Government Budget Speeches

2020

# Speech of Government Budget for the year 2020-2021

Tanzania, United Republic

Ministry of Finance and Planning

http://knowledgebank.mof.go.tz/handle/123456789/72

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2020/21

DODOMA MEI, 2020

# YALIYOMO

YALIYOMO ..... ii
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 MAJUKUMU YA WIZARA ..... 4
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA 2020/21 ..... 5
3.1 Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/20 ……5
3.2 Utekelezaji wa Majukumu ..... 8
3.2.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla 8
3.2.2 Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mikakati, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali.....10
3.2.3 Kubuni, Kuunda na Kusimamia Mifumo ya Usimamizi Fedha na Mali za Umma.....14
3.2.4 Usimamizi wa Sekta ya Fedha .....15
3.2.4.1 Taasisi za Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa.....17
3.2.4.2 Taasisi za Benki .....18
3.2.4.2.1 Benki za Maendeleo.....18
3.2.4.2.2 Benki za Biashara .....19
3.2.4.3 Taasisi za Bima .....19
3.2.4.4 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji.....20
3.2.5 Usimamizi wa Deni la Serikali.....21
3.2.6 Ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi .....22
3.2.7 Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma.....22
3.2.8 Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma 24
3.2.8.1 Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu .....24
3.2.8.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu .....25
3.2.9 Taasisi za Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma .....26
3.2.10 Mafao ya Wastaafu na Mirathi.....27

3.2.11 Tume ya Pamoja ya Fedha ..... 28
3.2.12 Sekta ya Michezo ya kubahatisha ..... 29
3.2.13 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ..... 29
3.3 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo ..... 31
3.3.1 Changamoto ..... 31
3.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto ..... 32
4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21 ..... 32
5.0 HITIMISHO ..... 34

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, iliyochambua bajeti za mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/21, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/21.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema pamoja na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka ujao wa fedha.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa kiongozi wetu, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kipindi chote cha muhula wa kwanza wa Serikali yake. Ni heshima kubwa kwangu kufanya kazi chini ya Kiongozi Mkuu wa nchi ambaye ana upeo mkubwa sana, mchapa kazi, mwenye uzalendo wa kweli na ambaye amestaajabisha Dunia kwa kutekeleza mambo makubwa ya kimaendeleo kwa kipindi kifupi. Itoshe tu kusema namshukuru sana, naendelea kumuombea afya njema yeye na familia yake ili kazi kubwa aliyoianza ya kuwaletea maendeleo makubwa

wananchi wa Tanzania iweze kukamilika. Ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania ni kuwa, nitaendelea kuchapa kazi katika kipindi chote cha utumishi wangu ili kuenzi nafasi hii adimu niliyokabidhiwa ya kutoa mchango wangu kwa mama Tanzania.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile**,** napenda nitumie jukwaa hili kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna walivyojitoa katika kuwahudumia Watanzania. Nimefurahi kufanya kazi chini yao na ninawasihi Watanzania kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaidizi hawa waandamizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni makini na wenye mapenzi ya dhati kwa nchi yao. Tuendelee kwa pamoja kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuwa na afya njema, hekima na busara katika kazi zao za kumsaidia Kiongozi Mkuu wa nchi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kusimamia muhimili huu wa Bunge kwa umahiri mkubwa sana. Aidha, ninakupongeza pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bajeti za Wizara mbalimbali. Naomba pia nitumie fursa hii kuishukuru kipekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb.), kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri waliyotupatia wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/21. Nakiri kwamba, mimi binafsi, Mhe. Ashatu K. Kijaji (Mb.) – Naibu Waziri na watendaji wa

Wizara yetu taasisi zake tumejifunza mambo mengi mazuri kutokana na hoja na ushauri wa Kamati hii nyeti. Vile vile, napenda nitumie fursa hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusimamia majukumu ya Wizara zao vizuri na kupelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 - 2020.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie pia nafasi hii kumpongeza sana *comrade* Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuwapoteza Mhe. Balozi Dkt Augustine Philip Mahiga (Mb.) aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Rashid Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini - CCM, Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliyekuwa Mbunge Viti Maalum – CCM na Mhe. Richard Mganga Ndassa (Senator) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve-CCM. Tunawaombea ili wapate rehema kwa Mungu, wapumzike kwa amani. Amina.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge makini wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nampongeza sana kwa uchapakazi na kujitoa kwake na napenda niwaombe Wananchi wa Jimbo la Kondoa wamrejeshe kwa kishindo mama huyu hodari katika Bunge lijalo. Aidha, nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali Bw.

Doto M. James na Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bw. Adolf H. Ndunguru na Bi. Mary N. Maganga kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vile vile, nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango (BoT, NBS, TR, CAG, TRA, TRAB, TRAT, Benki za Serikali, Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa, Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu) pamoja na watumishi wote wa taasisi hizo kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha utumishi wangu kama Waziri wa Fedha na Mipango.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu. Nitaanza kwa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/20, maeneo ya kipaumbele pamoja na mikakati mbalimbali ambayo itatekelezwa na Wizara kwa mwaka 2020/21. Aidha, nitawasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 kwa mafungu saba (7) ya Wizara ambayo ni Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 21 – HAZINA, Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili 2016, majukumu ya kisera na kiutendaji ya Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na:

i. Kubuni, kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera za fedha, bajeti, ununuzi wa umma na ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi;
ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mifumo, sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha na mali za umma;
iii. Kukusanya na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali;
iv. Kuandaa, kusimamia, kukagua, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango, Bajeti na Mikakati ya Maendeleo ya Taifa;
v. Kudhibiti na kusimamia ulipaji wa Deni la Taifa;
vi. Kudhibiti na kusimamia vitega uchumi vya Serikali pamoja na uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma;
vii. Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu;
viii. Kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi; na
ix. Kukusanya, kuchakata, kuandaa, kusambaza na kusimamia matumizi ya takwimu rasmi za Taifa.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MALENGO YA MWAKA 2020/21

### 3.1 Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/20

#### (i) Mapato

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi bilioni 967.04 kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwemo gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka

katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 626.57 sawa na asilimia 64.79 ya lengo.

**(ii) Matumizi**

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi trilioni 11.94** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu nane (8) ikijumuisha Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 11.21** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 730.58** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi bilioni 608.37** kwa ajili ya mishahara na **shilingi trilioni 10.60** matumizi mengineyo. Kati ya fedha zote za maendeleo, **shilingi bilioni 677.00** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 53.58** ni fedha za nje.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, mafungu ya Wizara yametumia jumla ya **shilingi trilioni 7.69** sawa na asilimia **64.40** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotumika, **shilingi trilioni 7.68** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 10.91** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **shilingi bilioni 186.99** kwa ajili ya mishahara na **shilingi trilioni 7.49** matumizi mengineyo. Kati ya fedha za maendeleo zilizotumika, **shilingi bilioni 3.90** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 7.01** ni fedha za nje. Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila Fungu ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.1 – 3.**

# Jedwali Na. 1:Fedha zilizotumika za Mishahara hadi Machi 2020.

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2019/20 | jumla ya kiasi kilichotumika hadi Machi, 2020 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Mishahara ya Idara/Vitengo | 8,132,510,000.00 | 5,603,095,944.01 | 69 |
| | | Ruzuku ya Mishahara Taasisi | 29,788,406,000.00 | 20,622,019,999.00 | 69 |
| 21 | HAZINA | Mishahara ya Idara/Vitengo | 5,658,915,000.00 | 3,703,970,274.26 | 65 |
| | | Ruzuku ya Mishahara Taasisi | 225,691,258,000.00 | 135,475,105,888.91 | 60 |
| | | Marekebisho ya Mishahara ya Watumishi wa Umma | 305,170,458,988.00 | - | 0 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | | 3,281,016,000.00 | 2,298,464,000 | 70 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 649,793,000.00 | 480,388,077.00 | 74 |
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 8,885,708,000.00 | 5,423,323,137.36 | 61 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 7,029,314,000.00 | 4,362,572,009.00 | 62 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | | 14,084,139,000.00 | 9,024,969,571.00 | 64 |
| **Jumla -Mishahara** | | | **608,371,517,988.00** | **186,993,908,900.54** | **31** |

# Jedwali Na. 2: Fedha zilizotumika za Matumizi Mengineyo hadi Machi 2020.

| Fungu | Jina la Fungu | | Bajeti iliyoidhinishwa 2019/20 | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi Machi 2020 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | | 9,721,127,000,000.00 | 7,198,596,718,311.79 | 74 |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | Uendeshaji wa Ofisi | 7,229,786,000.00 | 3,374,960,767.48 | 47 |
| | | Matumizi Maalum | 30,000,000,000.00 | 4,105,045,533.19 | 14 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | | 1,558,142,000.00 | 1,168,605,000.00 | 75 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | | 2,015,586,000.00 | 1,128,552,377.00 | 56 |
| 21 | HAZINA | Idara/Vitengo | 36,552,411,220.00 | 27,575,036,147.07 | 75 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 140,852,667,000.00 | 105,588,198,000 | 75 |
| | | Matumizi Maalum | 558,875,539,780.00 | 80,962,345,266.19 | 14 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | Idara/Vitengo | 23,313,168,000.00 | 18,789,291,600.43 | 81 |
| | | Ruzuku - Taasisi | 4,479,346,000.00 | 2,986,232,000.00 | 67 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | | 37,036,734,000.00 | 17,470,446,734.00 | 47 |
| 45 | Ofis ya Taifa ya Ukaguzi | | 40,992,739,000.00 | 32,161,747,099.00 | 78 |
| **Jumla - Matumizi Mengineyo** | | | **10,604,033,119,000.00** | **7,493,907,178,836.15** | **71** |

**Jedwali Na. 3:Fedha zilizotumika za Miradi ya Maendeleo hadi Machi 2020**

| Fungu | Jina la Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2019/20 | | Jumla ya kiasi kilichotumika hadi Machi, 2020 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,000,000,000.00 | 1,300,000,000.00 | 90,851,700.00 | 360,083,000.00 |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 200,295,998.00 | - | 173,054,011.50 |
| 21 | HAZINA | 656,000,000,000.00 | 27,717,888,733.00 | 137,005,000.00 | 3,074,164,240.44 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu | 2,000,000,000.00 | 1,300,000,000.00 | - | 722,930,000.00 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 13,000,000,000.00 | 21,763,757,000.00 | 2,196,828,476.25 | 2,092,161,495 |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 5,000,000,000.00 | 1,300,000,000.00 | 1,471,148,677.00 | 588,975,000 |
| **Jumla - Maendeleo** | | **677,000,000,000.00** | **53,581,941,731.00** | **3,895,833,853.25** | **7,011,367,746.94** |

## 3.2 Utekelezaji wa Majukumu

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kulieleza kwa ufupi Bunge lako Tukufu juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020.

### 3.2.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara iliweka malengo ya uchumi jumla kama msingi wa kubuni na kutunga sera zenye mwelekeo wa kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu. Malengo hayo ni pamoja na: kukuza Pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 7.1 kwa mwaka 2019; kudhibiti mfumuko wa bei ili kubaki katika wigo wa tarakimu moja na kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani ili kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa, mapato ya kodi asilimia 13.1 ya Pato la Taifa na nakisi ya bajeti asilimia 2.3 ya Pato la Taifa.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara ilichukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala ili kufikia malengo ya uchumi jumla. Miongoni mwa hatua

hizo ni pamoja na: kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kufanya Biashara nchini *(Blueprint)* ili kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi; kutumia sera ya riba ya Benki Kuu kutoa mwelekeo wa sera ya fedha; kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara; kununua fedha za kigeni katika soko la ndani; kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara kutoka asilimia 8 hadi asilimia 7; kuongeza wigo wa benki kutumia amana walizoweka Benki Kuu kutoka asilimia 10 hadi 20; kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma na kutoa fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati na ile ya kielelezo iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi za kisera na kiutawala zimeleta matokeo yafuatayo: kukua kwa Pato la Taifa kwa asilimia 7.0 mwaka 2019, kama ilivyokuwa mwaka 2018. Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo kwa mwezi Machi 2020, ulikuwa asilimia 3.4.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta zilizoongoza katika ukuaji ni pamoja na Uchimbaji wa Madini na Mawe asilimia 17.7, Ujenzi asilimia 14.1, Sanaa na Burudani asilimia 11.2; na Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo asilimia 8.7. Aidha, Ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mwaka 2019 ulikuwa kama ifuatavyo: Kenya asilimia 5.6; Uganda asilimia 4.9; na Rwanda asilimia 9.4.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** shabaha za uchumi jumla zinatarajiwa kuwa kama ifuatavyo: Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 4.0 mwaka 2020; mfumuko wa bei kubaki katika wigo wa tarakimu moja na nakisi ya bajeti ya Serikali kufikia asilimia 2.8, mapato ya ndani asilimia 14.5 ya Pato la Taifa na mapato ya kodi asilimia 12.5 ya Pato la Taifa. Matarajio haya ni kutokana na matokeo ya awali kufuatia athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (unaosababishwa na Virusi vya CORONA) kwenye sekta mbalimbali. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba, takwimu za mwenendo wa uchumi jumla zinapatikana kwa wakati ili kuiwezesha Serikali na wadau wengine kufanya maamuzi sahihi.

### 3.2.2 Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mikakati, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali

#### (i) Mpango wa Maendeleo wa Taifa

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa Tanzania inafikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Wizara inaendelea kusimamia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Agenda ya Afrika 2063. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21; kuandaa rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21; kuandaa andiko dhana la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; kuandaa taarifa ya Hiari ya Nchi Kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 *(SDGs*); kuunda mfumo wa kitaasisi wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za

utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 pamoja na mfumo wa awali (*prototype*) wa Kanzidata ya Kuhifadhi na Kutoa Taarifa za Miradi ya Maendeleo.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka ujao wa fedha 2020/21, Wizara imepanga kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17- 2020/21; kuandaa Mpango wa Maendeleo waTaifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na kukamilisha kazi ya kuandaa Kanzidata ya Kuhifadhi na Kutoa Taarifa za Miradi ya Maendeleo.

**(ii) Usimamizi wa Bajeti ya Serikali**

- **Mapato**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara ilipanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati mbalimbali ya kuongeza mapato. Sera na Mikakati hiyo ni pamoja na: Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi; kuhimizi matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika za Taasisiza Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa chache ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya taasisi za umma inawasilishwa kwa wakati; kuhakikisha kuwa maduhuli yote yanakusanywa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (*GePG*); kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kurekebisha viwango vya kodi kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji ili kulinda viwanda vya ndani. Hatua hizi pamoja na mikakati mingine zililenga kuiwezesha Serikali kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya **shilingi trilioni** 23.04.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi, pamoja na nyingine za usimamizi wa mapato, zimeiwezesha Serikali kukusanya mapato ya ndani jumla ya **shilingi trilioni 16.06** katika kipindi cha Julai 2019 na Machi 2020 sawa na asilimia 92.4 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia **shilingi trilioni 13.46** sawa na asilimia 94.7, mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.07** sawa na asilimia 84.4 na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **shilingi bilioni 527.3** sawa na asilimia 91.7. Mapato ya Ndani yameongezeka kwa asilimia 14.2 hadi **shilingi trilioni 16.06** kutoka **shilingi bilioni 14.07** kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia ilipanga kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu ya kiasi cha **shilingi trilioni 2.78** ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, fedha za misaada na mikopo nafuu zilizopokelewa zimefikia jumla ya **shilingi trilioni 2.04** sawa na asilimia 93 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, misaada iliyopokelewa ni **shilingi bilioni 853.06** sawa na asilimia 42, ambapo Misaada ya Kibajeti ni **shilingi bilioni 197.68,** Mifuko ya Kisekta **shilingi bilioni 202.99** na Miradi ya Maendeleo **shilingi bilioni 452.39.** Aidha, mikopo nafuu iliyopokelewa ni **shilingi trilioni 1.18** sawa na asilimia 58. Kati ya fedha za mikopo nafuu zilizopokelewa, Mifuko ya Kisekta imepokea **shilingi bilioni 39.41** na Miradi ya Maendeleo **shilingi trilioni 1.14.**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikisha mkopo wa kiasi cha **shilingi trilioni 3.44** kutoka katika soko la ndani, sawa na asilimia 101.5 ya lengo la kukopa **shilingi trilioni 3.39** katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, fedha **shilingi**

**trilioni 2.58** zimetumika katika kulipa deni la mikopo ya ndani iliyoiva na **shilingi bilioni 860.6** zimetumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, hadi kufikia Machi 2020, **shilingi trilioni 1.82** zimekopwa kutoka soko la nje sawa na asilimia 78.45 ya lengo la kukopa **shilingi trilioni 2.32.**

- **Matumizi**

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, Wizara imekasimiwa jukumu la kutoa, kusimamia, kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, jumla ya **shilingi trilioni 24.65** zilitolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Katika kipindi hicho, **shilingi trilioni 1.16** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na **shilingi bilioni 597.54** kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa ya wakandarasi (**shilingi bilioni 247.50**), wazabuni (**shilingi bilioni 147.73**), watumishi (**shilingi bilioni 97.62**), madeni mengineyo (**shilingi bilioni 88.87**) na watoa huduma (**shilingi bilioni 15.82**). Aidha, jumla ya **shilingi bilioni 33.98** sawa na asilimia 84.95 ya bajeti iliyotengwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya kimkakati inayotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa Mikakati, Mipango na Bajeti ya Serikali katika mwaka 2020/21, Wizara inatarajia kufanya yafuatayo: kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17- 2020/21; kuandaa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;

kuanza maandalizi ya kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo; kuunda, kuhuisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali; kutekeleza hatua za kibajeti na za kifedha za kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji; kuandaa Miongozo, Mikakati na Mipango ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22; kuandaa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma; na kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu ukusanyaji wa maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau ili kuangalia uwezekano wa kutunga sera ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na mkakati wa utekelezaji ikiwa ni mkakati wa kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali.

### 3.2.3 Kubuni, Kuunda na Kusimamia Mifumo ya Usimamizi Fedha na Mali za Umma

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanya yafuatayo: kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (*GePG*) kwa kuwezesha kupatikana kwa huduma kwa njia ya simu ya kiganjani (*GePG application mobile*) na kwa kuunganisha mfumo huu na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ya ukusanyaji wa mapato. Aidha, katika kipindi hicho, taasisi 158 zimeunganishwa kwenye mfumo wa *GePG* na kufanya jumla ya Taasisi zilizounganishwa kufikia **632**. Wizara inaendelea na zoezi la kuunganisha Taasisi 35 zilizobaki na kuendesha mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo kwa taasisi za umma ili kufikia azma ya Serikali ya kuunganisha taasisi zote ifikapo Juni 2020.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na**:** kubuni na kuanzisha mfumo wa Usimamizi wa shughuli za Kihasibu na Malipo katika Taasisi za Umma - MUSE; mfumo wa kuratibu Usimamizi na Utoaji wa Misamaha ya Kodi; mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Misaada zinazoelekezwa moja kwa moja kwenye miradi bila kupita kwenye mifumo ya Serikali – D-fund; mfumo wa Utoaji Leseni za Udalali na Uendeshaji wa Minada na mfumo wa Usajili wa Huduma na Watoa Huduma za Fedha (*Financial Service Registry*).

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kubuni, kuunda na kuhuisha mifumo ya usimamizi wa fedha na mali za umma kulingana na mahitaji pamoja na mabadiliko ya kiteknolojia. Aidha, Wizara itajielekeza katika kutoa mafunzo, hususan matumizi ya mifumo iliyoundwa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha na mali za Serikali. Vile vile, mifumo hii, pamoja na mambo mengine, itatumika kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza na zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya Serikali. Katika udhibiti na usimamizi wa fedha na mali za Serikali, mifumo hii itaokoa muda wa uendeshaji na usimamizi pamoja na kurahisisha upatikanaji wa taarifa, ikiwa ni pamoja na taarifa zinazohusu miamala shuku na ufadhili wa ugaidi.

### 3.2.4 Usimamizi wa Sekta ya Fedha

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu hili linatekelezwa kwa kuandaa, kutunga na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu za sekta ya fedha, ikiwemo

masoko ya mitaji na dhamana pamoja na bidhaa. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inashirikiana na Taasisi na Mamlaka za Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Fedha ambazo ni Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania; Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana; Soko la Hisa la Dar es Salaam; Soko la Bidhaa Tanzania -TMX; Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja – UTT na Mfuko wa SELF- *Microfinance*.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikiwa kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 ambazo zilianza kutumika rasmi mwezi Novemba 2019. Aidha, katika kuhakikisha kuwa wadau wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sera, sheria na kanuni za sekta ya huduma ndogo za fedha, Wizara imeanza utekelezaji wa Mpango Maalum wa Elimu kwa Umma kuhusu sekta hii. Vile vile, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha; Kanuni za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha; na kufanya utafiti wa Mchango wa Mikopo ya Nyumba (*Housing Mortgage Finance*) katika kukuza uchumi.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, kukamilika kwa nyaraka hizi, kutaongeza uelewa katika jamii kuhusu mambo ya msingi ya kuzingatia katika utoaji wa huduma ndogo za fedha, umuhimu wa sekta ya fedha na huduma jumuishi za fedha pamoja na mchango wa sekta ya fedha katika ukuaji wa shughuli za kiuchumi na maendeleo ya watu.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zilizochukuliwa katika utekelezaji wa sera ya fedha ni pamoja na: kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara; kununua fedha za kigeni katika soko la ndani; kuzipunguzia benki

za biashara kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu kutoka asilimia 8 hadi asilimia 7; kuongeza wigo wa benki kutumia amana walizoweka Benki Kuu kutoka asilimia 10 hadi 20 mwezi Julai 2019; kuridhia mfumo wa kisheria wa makubaliano ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi baina ya benki (*Global Master Repurchase Agreement - GMRA*) ili kuongeza ufanisi na ukwasi katika masoko ya fedha. Hatua hizi kwa pamoja zimesaidia kuongeza kiwango cha ukwasi katika uchumi na kusababisha wastani wa amana za benki za biashara katika Benki Kuu (*clearing balances*) kufikia shilingi bilioni 628.8 kati ya Julai 2019 na Machi 2020 ikilinganishwa na wastani wa shilingi bilioni 462.7 kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Vile vile, wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ulifikia asilimia 9.0 ikilinganishwa na asilimia 6.1 kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

#### 3.2.4.1 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - *CMSA* na Soko la Bidhaa Tanzania – *TMX* zimepewa jukumu la kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa. Nyaraka zilizoandaliwa na kuanza kutumika katika eneo hili ni pamoja na: Mwongozo wa Mfumo wa Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana unaozingatia vihatarishi (*Risk Based Supervision Guideline)*; programu maalum ya kuziwezesha kampuni ndogo ndogo kukuza mitaji na kuvutia uwekezaji DSE (*Enterprise Acceleration Program*) na Kanuni Mpya za Uendeshaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam – *DSE Rules* ili kuongeza uwazi katika shughuli za minada ya dhamana.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - *CMSA* kwa kushirikiana na Soko la Hisa la Dar es Salaam – *DSE* ilifanikisha kuidhinishwa kwa hatifungani ya Benki ya Biashara ya NMB yenye thamani ya shilingi bilioni 83.30, sawa na asilimia 333 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 25. Aidha, Soko la Hisa la Dar es Salaam limefanikiwa kukamilisha usajili wa kudumu wa Shirikisho la Masoko ya Hisa Duniani (*World Federation of Exchanges- WFE*) na kupata hadhi ya *Classification Frontier Market Status*.

### 3.2.4.2 Taasisi za Benki

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia taasisi za benki zikiwemo za maendeleo na biashara. Taasisi hizi ni mahsusi kwa ajili ya kutoa mikopo ya kibiashara na uwekezaji ya muda mfupi, wa kati na mrefu; na kupokea amana.

#### 3.2.4.2.1 Benki za Maendeleo

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** benki za maendeleo zinajumuisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB na Benki ya Maendeleo TIB. Kati ya mwezi Julai 2019 na Machi 2020, benki za maendeleo zimetoa mikopo ya jumla ya **shilingi bilioni 54.44** sawa na asilimia 32.9 ya kutoa mikopo ya **shilingi bilioni** 164.84. Kati ya kiasi hicho, Benki ya Kilimo Tanzania ilitoa mikopo yenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 35.86** sawa na ufanisi wa asilimia 176.3 ya lengo la kukopesha **shilingi bilioni 20.34** na benki ya TIB **shilingi bilioni 18.58** sawa na asilimia **12.86** ya lengo la kukopesha **shilingi bilioni 144.5**. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: kilimo, maji, utalii, viwanda vya kuchakata mazao, elimu, makazi, biashara, huduma nyinginezo na madini hususani madini

ya ujenzi. Jumla ya miradi iliyonufaika na mikopo hiyo ilikuwa 46. Kati ya miradi hiyo, miradi 38 imefadhiliwa na benki ya TADB na miradi 8 imefadhiliwa na benki ya TIB.

#### 3.2.4.2.2 Benki za Biashara

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** benki za biashara zinazosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango ni Benki ya Biashara TIB na TPB. Kati ya Julai 2019 na Machi 2020, benki za biashara zimefanikiwa kukusanya amana za jumla ya **shilingi bilioni 730.14** na kutoa mikopo yenye thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 631.94**. Kati ya kiasi hicho, benki ya TIB ilikusanya amana za jumla ya **shilingi bilioni 295.14** na kutoa dhamana na mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 188.94**. Aidha, benki ya TPB ilikusanya amana za jumla ya **shilingi bilioni 435** na kutoa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 443**. Maeneo yaliyonufaika na dhamana na mikopo hiyo ni pamoja na: Kilimo, biashara, fedha, uvuvi, viwanda, afya, na ujenzi. Vile vile, benki ya TPB imefanikiwa kutoa gawio la jumla ya **shilingi bilioni 1.5** kwa wanahisa wake.

### 3.2.4.3 Taasisi za Bima

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Bima Tanzania – TIRA pamoja na Shirika la Taifa la Bima – NIC ndiyo taasisi pekee za Serikali zinazotoa huduma za bima hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Mamlaka ya Bima Tanzania imefanikiwa kuandaa Mwongozo na Taratibu za Fidia kwa wateja wa kampuni za bima pamoja na Mkakati wa Kumlinda Mteja na Mtumiaji wa Huduma za Bima. Aidha, Wizara imeliondoa Shirika la Taifa la Bima kwenye orodha ya mashirika yanayotakiwa kubinafsishwa ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ili kukidhi mahitaji ya soko, NIC imeanza kujenga mfumo wa

Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Bima ili kujenga mazingira wezeshi na shindani. Mfumo huu utaongeza uwazi na kuwawezesha wateja kuwasilisha madai yao kwa njia ya mtandao.

### 3.2.4.4 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Mipango inasimamia mifuko miwili ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ni Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS na Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (*Self Microfinace Fund)*. Katika mwaka 2019/20 UTT AMIS imeanzisha Mfuko wa Hatifungani uliozinduliwa mwezi Septemba 2019, ambapo thamani ya Mfuko imefikia **shilingi bilioni 34.6** na wanachama **2,917** mwezi Machi 2020. Aidha, hadi kufikia Machi 2020, UTT AMIS iliuza vipande vya mifuko na huduma ya usimamiaji mitaji (*wealth management*) vyenye thamani ya **shilingi bilioni 101.26** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 36** katika kipindi kama hicho mwaka 2019. Vile vile, thamani ya vipande vya mifuko iliongezeka kwa **shilingi bilioni 25.43**, rasilimali za mifuko **shilingi bilioni 76.68** na idadi ya wawekezaji iliongezeka kutoka wawekezaji **145,773** hadi **157,339** sawa na ongezeko la asilimia **7.9**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu huduma za kununua na kupata taarifa za vipande zinapatikana kwa kutumia simu za mkononi.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2020, Mfuko wa SELF umetoa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 29.83** sawa na asilimia **81** ya lengo la mwaka na kiwango cha urejeshaji wa mikopo kilifikia asilimia **95**. Kiasi hicho cha mikopo kimetolewa kwa wajasiriamali wadogo **8,705** wanaojishughulisha na shughuli za kilimo, viwanda vidogo pamoja na biashara ndogo ndogo. Mikopo katika

sekta ya kilimo ilielekezwa katika uzalishaji, pembejeo, zana za kilimo pamoja na mnyororo wa thamani. Aidha, kwa upande wa viwanda vidogo, mikopo ilielekezwa katika kutengeneza mashine za kuzalisha sabuni na kukamua mafuta ya alizeti na mawese.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kuandaa sera, sheria, kanuni, mifumo ya TEHAMA, mikakati, miongozo na taratibu mbalimbali za kusimamia na kuendeleza sekta ya fedha, ikiwa ni pamoja na: Sera Maendeleo ya Sekta ya Benki, Masoko ya Mitaji na Dhamana pamoja na Bima. Aidha, Wizara inatarajia kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mikopo Salama, kufanya mapitio ya Sheria ya Bima ya Mwaka 2009 na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 pamoja na kanuni zake ili kuendana na sera mpya zinazotarajiwa kuandaliwa.

### 3.2.5 Usimamizi wa Deni la Serikali

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134. Kipaumbele ni kukopa kutoka kwenye vyanzo vyenye masharti nafuu na fedha zinazopatikana kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo, hususan miradi inayochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na maendeleo ya watu. Vile vile, Wizara inaendelea kuhakikisha kuwa, madeni yote yanayoiva yanalipwa kwa wakati.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Serikali ilifanikiwa kulipa deni lake lote lililoiva lenye thamani ya **shilingi trilioni 6.19**. Kati ya kiasi hicho, Deni la Ndani ni **shilingi trilioni 4.06** ikijumuisha riba **shilingi**

**trilioni 1.08** na mtaji **shilingi trilioni 2.98**. Aidha, Deni la Nje ni **shilingi trilioni 2.13** ikijumuisha riba ya **shilingi bilioni 636.75** na mtaji **shilingi trilioni 1.49.**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2020/21, Wizara itaandaa na kutekeleza mikakati itakayowezesha Serikali kukopa katika soko la fedha la ndani na nje bila kuathiri uhimilivu wa deni la Serikali, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134 na vigezo vya viashiria hatarishi vya madeni yaliyotokana na dhamana za Serikali.

### 3.2.6 Ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikisha kutungwa kwa Kanuni za Sheria ya Ubia za Mwaka 2020 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.37. Aidha, Wizara imeendelea kupokea, kuchambua na kutoa ushauri kwa Mamlaka za Serikali zinazotekeleza miradi **10** ya PPP ambayo ipo katika hatua za awali za kutafuta wabia, washauri elekezi, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inatarajia kukamilisha taratibu za kuanzisha kituo cha ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *PPP Center*. Aidha, Wizara itaendelea kupokea na kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya ubia itakayowasilishwa na Taasisi na Mashirika ya Umma na kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wadau wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi.

### 3.2.7 Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kusimamia vitega uchumi, Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na kampuni binafsi ambazo

Serikali ina hisa chache. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanikiwa kujenga Mfumo wa TEHAMA wa kutunza na kusimamia taarifa za wajumbe wa bodi za Mashirika na Taasisi ujulikanao kama *Board Management Information System* ili kurahisisha kazi ya usimamizi, ufutiliaji na tathmini. Katika kipindi hicho, Serikali ilifanikiwa kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 612.87** kutoka kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kama gawio na michango ya Mashirika kwenye Mfuko Mkuu.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya kazi ya ufuatiliaji na tathmini ya vitega uchumi vilivyobinafsishwa yanaonesha kuwa hoteli na nyumba za kulala wageni zimeajiri idadi kubwa ya Watanzania, zinalipa kodi na kuzingatia Sera ya Kulinda Mazingira. Hata hivyo, baadhi ya wawekezaji wa hoteli na nyumba za kulala wageni hawazingatii masharti ya mikataba ya mauzo, ikiwemo kutokuwa na mipango endelevu ya uwekezaji. Wizara itaendelea kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa, vitega uchumi vya Serikali vilivyobinafsishwa vinaendeshwa kwa mujibu wa mikataba.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma, Wizara inatarajia kufanya yafuatayo katika mwaka 2020/21: kufanya ufuatiliaji na tathmini wa kampuni tanzu za mashirika na taasisi za umma ili kubainisha na kujiridhisha kama zinaendeshwa kwa tija, malengo ya uanzishwaji wake na kubaini ziada ya mapato na michango inayostahili kuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanya mapitio ya Sheria na Muundo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha usimamizi wa uwekezaji wa Serikali katika Mashirika na Taasisi za Umma, Kampuni Tanzu

pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

### 3.2.8 Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Taasisi tano (5) za mafunzo ya elimu ya juu na Bodi mbili (2) za kitaaluma ambazo ni: Chuo cha Usimamizi wa Fedha -IFM; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP; Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA; Chuo cha Uhasibu Arusha –IAA; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC; Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA. Taasisi hizi zinatoa mafunzo, kuendeleza wataalamu na wanataaluma, kufanya tafiti, na kutoa ushauri wa kitaalamu katika tasnia ya mipango, kodi, usimamizi wa fedha, takwimu na ununuzi na ugavi.

#### 3.2.8.1 Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2019/20; taasisi za mafunzo ya elimu ya juu zimedahili jumla ya wanafunzi **44,511** ikiwa ni ongezeko la wanafunzi **5,286** ikilinganishwa na wanafunzi **39,225** waliodahiliwa mwaka 2018/19. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi waliodahiliwa kwa ngazi ya cheti ni **12,714**, stashahada **9,941**, shahada **21,044** na uzamili **812**. Takwimu hizo zinaonesha kuwa, kuna ongezeko la mahitaji na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kozi za mipango, uhasibu, takwimu na ununuzi na ugavi.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wanafunzi, Wizara inafanya jitihada za kuongeza nafasi za udhamini wa Wahadhiri kwa ngazi ya uzamivu na uzamili katika vyuo vya ndani na nje ya nchi

pamoja na kuboresha miundombinu ya kufundisha na kujifunza. Katika mwaka 2019, jumla ya Wahadhiri **91** wamepewa udhamini wa kujiendeleza na kati ya hao, Wahadhiri **77** ni ngazi ya uzamivu na **14** uzamili. Aidha, Taasisi zinatekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya madarasa, mabweni na majengo ya utawala ili kukabiliana na changamoto ya upungufu na uchakavu wa miundombinu hiyo. Chuo cha IFM kinaendelea na Ujenzi wa Kampasi ya Kanda ya Ziwa, Simiyu; Chuo cha IRDP kinakamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike Kampasi Kuu Dodoma na Chuo cha Uhasibu Arusha kimekamilisha ukarabati wa madarasa.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Taasisi za Mafunzo ya Elimu ya Juu zinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi **61,827** katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada, uzamili na uzamivu. Aidha, Wahadhiri **138** wanatarajia kupata udhamini katika ngazi ya uzamili na uzamivu katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Wahadhiri **22** watapata udhamini katika ngazi ya uzamili na **116** uzamivu.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, chuo cha IFM kitaendelea na kazi ya Ujenzi wa Kampasi ya Kanda ya Ziwa - Simiyu na Chuo cha IRDP kinatarajia kuanza ujenzi wa madarasa, bweni la wanafunzi na ofisi ya Kampasi ya Kanda ya Ziwa - Mwanza. Aidha, Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha SURA 91 itafanyiwa mapitio ili kuendana na mabadiliko ya mifumo ya elimu ya juu, soko, uchumi na teknolojia.

### 3.2.8.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2020, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB imefanikiwa kufanya yafuatayo: kusajili jumla ya

wataalamu wapya **632**, na Taasisi mbili (2); na kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa taasisi mbalimbali.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Julai 2019 na Machi 2020, Bodi ya NBAA imefanikiwa kusajili watunza vitabu (*Accounting Technicians or equivalent*) watatu (3), wahasibu wahitimu wanaopatiwa uzoefu wa kazi **376**, wahasibu ngazi ya CPA **88**, wakaguzi hesabu katika ngazi ya CPA-PP **35** (*Auditors*), kampuni za ukaguzi wa hesabu **13** na kampuni za uhasibu sita (**6**). Aidha, Bodi imetoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi kwa taasisi za Umma na binafsi tisa (**9**); kutoa machapisho ya vitabu vya rejea kwa watahiniwa wa Uhasibu pamoja na Jarida la Wahasibu na Wakaguzi Hesabu na kufanya ukaguzi wa kampuni **43** za uandaaji na ukaguzi wa hesabu.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Bodi ya PSPTB na NBAA zitaendelea kudahili na kuendesha mitihani ya kitaaluma na kitaalamu; kufanya tafiti; kujenga uwezo wa wataalamu; kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi; kusimamia ubora wa kazi za wataalamu na wanataaluma pamoja na kufanya usajili wa wataalamu wa fani ya Uhasibu, Ukaguzi wa Hesabu na Ununuzi na Ugavi. Aidha, Bodi ya NBAA chini ya usimamizi wa Wizara inakamilisha mapitio ya sheria yake ili kuwezesha kutungwa kwa Sheria mpya ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ili kukidhi mahitaji ya soko na mabadiliko ya kitaalamu, kitaaluma, kiuchumi na kiteknolojia.

### 3.2.9 Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utatuzi wa migogoro ya kodi na ununuzi wa umma kupitia Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Ununuzi

wa Umma – PPAA, Bodi ya Rufani za Kodi- TRAB na Baraza la Rufani za Kodi-TRAT.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuziwezesha kibajeti na rasilimali watu Mamlaka za Rufani za Kodi na Ununuzi ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya Julai na Machi 2020, TRAB imesikiliza mashauri **407** yenye thamani ya **shilingi trilioni 1.16** na **dola za Marekani milioni 71.80**. Aidha, kwa sasa TRAB inaendelea kusikiliza mashauri **447** ya kodi yaliyorundikana kwa utaratibu maalumu (*special sessions*). Vile vile, kati ya Julai 2019 na Machi 2020, PPAA ilipokea, kusikiliza na kutolea maamuzi jumla ya mashauri **20**.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kuziwezesha Taasisi za Rufani za Kodi na Ununuzi ili kusikiliza mashauri ya wadau kwa wakati na hivyo kuiwezesha Serikali kufanikisha azma yake ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara. Aidha, Wizara itaiwezesha TRAB na TRAT kukarabati jengo la ofisi ili kukabiliana na changamoto ya mazingira ya kufanya kazi.

### 3.2.10 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inawajibika kulipa mafao na pensheni kwa watumishi wa Umma ambao hawachangii katika mifuko ya hifadhi ya jamii, mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa. Kati ya mwezi Julai 2019 na Machi 2020, Wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali **57,605**, mirathi kwa warithi **1,006** na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi **457** wa Serikali walio kwenye mikataba. Aidha, Wizara imeendelea kufanya uhakiki wa Daftari la Pensheni kila

mwezi kabla ya malipo; kuandaa vitambulisho vipya vya wastaafu vya kielektroniki katika mfumo wa "*smart cards*" na kuboresha Mfumo wa unaotumika kutoa huduma kwa njia ya mtandao na kudhibiti fedha za mirathi zinazotoka HAZINA kwenda moja kwa moja kwenye akaunti za warithi (*Tanzania Pensioners Payment System – TPPS).*

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kutoa huduma za pensheni, mirathi, utunzaji wa kumbukumbu (masijala) na uhakiki wa wastaafu kwa njia ya mtandao na kuwapatia Wastaafu vitambulisho vya kielektroniki.

### 3.2.11 Tume ya Pamoja ya Fedha

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Pamoja ya Fedha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri juu ya masuala ya uhusiano wa kifedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika mwaka 2019/20, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya stadi kuhusu Mfumo wa Biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar na Mwenendo wa Mapato ya Muungano. Aidha, Tume imefanya uchambuzi wa taarifa na takwimu halisi za Mapato na Matumizi ya Muungano kwa mwaka 2017/18 na Bajeti ya mwaka 2018/19 na 2019/20. Taarifa ya uchambuzi wa takwimu hizo ilijadiliwa na Sekretarieti ya Tume mwezi Februari, 2020 na Serikali za pande zote zinaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Tume ya Pamoja ya Fedha inatarajia kufanya Stadi kuhusu mwenendo wa ukuaji wa sekta za uchumi na mapato ya Muungano na kukusanya na kufanya uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji

wa mambo ya Muungano.

### 3.2.12 Sekta ya Michezo ya kubahatisha

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iliendelea kuboresha mazingira ya kuendeleza tasnia ya michezo ya kubahatisha pamoja na kuimarisha mifumo ya uendeshaji na udhibiti wake. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Wizara imefanikisha kazi ya marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha SURA 41 ili kuipa Bodi mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kudhibiti matangazo ya michezo ya kubahatisha. Aidha, Bodi imeunda mifumo miwili ya uendeshaji na udhibiti wa michezo ya kubahatisha ambayo ni mfumo wa kutoa leseni, ukaguzi na uzingatiaji *(Gaming Licensing, Inspection and Compliance Application - GLICA)* na mfumo wa ufuatiliaji wa michezo ya kubahatisha (*Gaming Regulatory Monitoring System – GREMS)*.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imepanga kuimarisha usimamizi na kuongeza udhibiti wa michezo ya kubahatisha kwa kuunganisha mifumo ya uendeshaji na Mfumo wa Ulipaji Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mfumo wa Usajili wa Kampuni, Mfumo wa Ufuatiliaji wa Miamala ya Kampuni za Simu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - pamoja na Mfumo wa Vitambulisho vya Taifa. . Aidha, Mfumo wa kudhibiti Mashine za Slots - SIGMa utasimikwa ili kuimarisha mazingira ya udhibiti wa mashine hizo.

### 3.2.13 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kitengo cha Udhibiti Fedha

Haramu kilipokea na kuchambua taarifa za miamala shuku 724 kati ya mwezi Julai 2019 na Machi 2020. Kati ya miamala hiyo, taarifa fiche 61 zimewasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, Kitengo kimeingia makubaliano na Vitengo vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Japan na Jamhuri ya Kongo kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya kimataifa ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Kitengo kinatarajia kuboresha na kuhuisha mifumo ya upokeaji wa taarifa za miamala shuku na kusimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa matokeo ya tathmini ya kitaifa ya mifumo ya kudhibiti utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

### 3.2.14 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwenye matumizi ya rasilimali za umma, hadi kufikia Machi 2020, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi kwa mafungu **66** ya Wizara na Idara za Serikali; Wakala **33**; Taasisi **48**; Balozi **42**; Vyama vya Siasa **19**; Bodi za Mabonde ya Maji **14**; Hospital za Rufaa **27**, Mashirika ya Umma **150**; Mamlaka za Serikali za Mitaa **185**; Mikoa **26**; na Mifuko Maalumu **16**. Aidha, ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ya ujenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **19**. Vile vile, ukaguzi umefanyika kwa miradi ya maendeleo **435** ikijumuisha miradi **65** ya Serikali Kuu na miradi **370** ya Serikali za Mitaa.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepanga kuimarisha ukaguzi wa Miradi

ya Maendeleo hadi ngazi za Tarafa, Kata na Vijiji; kufanya ukaguzi wa miradi mikubwa ya maendeleo (Reli ya Kisasa, Vivuko, Bomba la Gesi Mtwara na Ukarabati wa Reli ya Kati); kupanua mawanda ya ukaguzi katika eneo la uchimbaji wa madini, mafuta na gesi ikiwemo kuimarisha ukaguzi wa kiuchunguzi na kiufundi; na kuendelea kufanya ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma pamoja na kufanya ukaguzi wa ufanisi.

## 3.3 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliana nazo

### 3.3.1 Changamoto

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya Wizara unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo tunaendelea kukabiliana nazo kwa kushirikiana na wadau wengine ili zisilete athari hasi katika malengo tuliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:

(i) Kasi ndogo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(ii) Mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayoleta uhitaji wa upatikanaji wa teknolojia mpya na kuboresha na kuhuisha teknolojia ya mifumo iliyopo ili kuongeza ufanisi;

(iii) Kuongezeka kwa gharama za mikopo kwenye masoko ya fedha duniani kutokana na mabadiliko ya sera za fedha katika nchi zilizoendelea (hususan Marekani na Nchi za Ulaya);

(iv) Uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja kutokana na mafuriko; na

(v) Mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).

### 3.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na:

(i) Kutunga sera na mkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za maendeleo;

(ii) Kujenga uwezo wa wataalam wa ndani katika kubuni, kuunda na kuhuisha teknolojia ya mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato;

(iii) Kuhamasisha wadau wa ndani kuendelea kushiriki katika minada ya dhamana za Serikali pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya mikopo ya nje vyenye riba nafuu; na

(iv) Wizara inakamilisha uchambuzi wa taarifa mbalimbali za kisekta ili kubaini kiwango cha athari zitokanazo na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) katika uchumi na kuainisha mikakati ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya kukabiliana nazo.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/21

### (i) Makadirio ya Mapato

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya kiasi cha **shilingi bilioni 973.02** kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni

pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa na mafungu ya Wizara ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa na Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango katika mwaka 2020/21**

| Fungu | Jina la Fungu | Kiasi |
|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 931,065,159,090 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 41,791,905,888 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 158,000,000 |
| **JUMLA** | | **973,015,064,978** |

**(ii) Makadirio ya Matumizi**

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi trilioni 12.39** kwa mafungu yote saba (7) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 11.73** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 659** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida, **shilingi trilioni 10.48** kwa ajili ya deni la Serikali, **shilingi bilioni 750.29** matumizi mengineyo na **shilingi bilioni 510** kwa ajili ya mishahara na marekebisho ya mishahara. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi bilioni 624.7** fedha za ndani na **shilingi bilioni 34.61** fedha za nje.

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 80.54** kwa ajili ya matumizi ya kawaida

na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 68.87** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 11.67** matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi bilioni 14.88** kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 53.99** matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi bilioni 6.70** fedha za ndani na **shilingi bilioni 4.97** fedha za nje. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2020/21**

| FUNGU NA. | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA-MATUMIZI YA KAWAIDA | NDANI | NJE | JUMLA-MAENDELEO | |
| 7 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 3,375,080,000 | 22,229,786,000 | 25,604,866,000 | 1,000,000,000 | 1,300,000,000 | 2,300,000,000 | 27,904,866,000 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 802,823,000 | 2,048,142,000 | 2,850,965,000 | - | - | - | 2,850,965,000 |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu | - | 2,915,586,000 | 2,915,586,000 | - | 500,000,000 | 500,000,000 | 3,415,586,000 |
| 21 | HAZINA | 450,901,950,000 | 637,275,862,000 | 1,088,177,812,000 | 616,196,465,000 | 24,807,427,000 | 641,003,892,000 | 1,729,181,704,000 |
| 22 | Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo | 9,989,416,000 | 10,477,797,406,000 | 10,487,786,822,000 | - | - | - | 10,487,786,822,000 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 5,738,683,000 | 58,036,734,000 | 63,775,417,000 | 2,000,000,000 | 1,500,000,000 | 3,500,000,000 | 67,275,417,000 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 39,237,998,000 | 27,792,514,000 | 67,030,512,000 | 5,508,880,000 | 6,507,551,000 | 12,016,431,000 | 79,046,943,000 |
| **JUMLA - MAFUNGU YA WIZARA** | | **510,045,950,000** | **11,228,096,030,000** | **11,738,141,980,000** | **624,705,345,000** | **34,614,978,000** | **659,320,323,000** | **12,397,462,303,000** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 14,883,256,000 | 53,993,739,000 | 68,876,995,000 | 6,700,000,000 | 4,967,940,000 | 11,667,940,000 | 80,544,935,000 |

## 5.0 HITIMISHO

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyotangulia kusema, Mkutano huu wa Bunge ni wa mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kutumia fursa hii kukiri kuwa, katika kipindi chote cha muhula huu, Wizara imenufaika sana na maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao umesaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na

kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa namna ya pekee, naomba nirudie tena kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuongoza Bunge hili kwa umakini na umahiri mkubwa.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine, naomba nirudie kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuifanya kazi yake ya Waziri wa Fedha na Mipango aliyonipa kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ngumu kwa miaka mitano mfululizo. Vile vile, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania, hususan kwa kufanya kazi na kulipa kodi ili kujenga uchumi wa nchi yetu. Nawaomba Watanzania tuendelee kuchapa kazi kama anavyotuasa Mheshimiwa Rais wetu na kuitekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya "HAPA KAZI TU".

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na janga la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19), napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na madhara yanayotokana janga hili na kuwaasa kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa huu kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya. Aidha, napenda kuwapongeza kwa dhati madaktari na watumishi wote wa Afya walio mstari wa mbele siku zote katika kutoa huduma kwa wananchi, hasa wanyonge na hususan katika kipindi hiki cha mlipuko wa COVID-19 nchini.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa

kunisikiliza. Aidha, nawashukuru wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mof.go.tz.*

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.